**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**


***Namba za Simu***
*Mkuu wa Shule:* ***0754486342***
*Makamu Mkuu wa Shule**: 0769178802***
*Mtaaluma:* ***0786905178***
*Malezi:* ***0787443482***

**Shule ya Sekondari Loliondo,**
**S.L.P. 61,**
**LOLIONDO.**


**Tarehe: 24/04/2024**

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi
…………………………………………….
S.L.P ………………….………………..
……………………...………………..

## YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LOLIONDO HALMASHAURI YA NGORONGORO MKOA ARUSHA MWAKA 2024

1.0 Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2024. Shule ya Sekondari Loliondo ipo umbali wa Kilometa **420** Kaskazini mwa mji wa **ARUSHA** usafiri wa basi kutoka mjini **ARUSHA** Unapatikana katika kituo cha mabasi **Uwanja wa Mpira wa Sheikh Amri Abeid Amani Karume** au **Stand ya Dar express** nauli ni shilingi 23,000/=

Muhula wa masomo unaanza tarehe 01/07/2024. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 01/07/2024. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 14/07/2024.

### 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 **SARE YA SHULE**

(i) Sare ya shule ni suruali 02 za Dark Blue (kitambaa cha esteem) suruali iwe na marinda mbele na isiyo bana mwili ifunike kamba za viatu, makoti 02 yanayoendana na rangi ya suruali – dark blue – litavaliwa kama sare ya shule. Lisiwe la mtumba na shati jeupe la mikono mirefu.
(ii) Sare ya michezo kwa shule hii ni track-suit ya rangi ya njano, Bukta ya michezo rangi ya njano (Deep yellow) na raba nyepesi.
(iii) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na gidamu vyenye visigino vifupi.
(iv) Soksi jozi mbili nyeupe
(v) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi wenye 'buckle' ya chuma.
(vi) Masweta 2 ya rangi ya Dark Blue
(vii) Nguo za kushindia (shamba dress) suruali ya khaki yenye sifa kama ilivyo elekezwa katika sare ya darasani.
(viii) T-shirt 2 za rangi ya kijivu zisizo na maandishi yoyote (shingo ya "round") zinapatikana kwenye maduka yaliyopo karibu na shule.
(ix) Tai ya rangi ya Dark Blue

(x) Koti refu Jeupe (kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi)




**2.2 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI NI:-**

(i) Ream ya karatasi 1 (kwa mwaka)
(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
(iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
(iv) Scientific calculator na Oxford Advanced Learner's Dictionary.
(v) Godoro kwa wanafunzi wa bweni futi $2^{1}/_{2}$
(vi) Mashuka ya rangi ya Bluu Bahari (Light Blue) pair 2, blanket 1, foronya 1, chandarua 1
(vii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe), vyombo vya plastiki na bati ni marufuku.
(viii) Ndoo moja ya  lita 20 yenye mfuniko
(ix) Brashi ya chooni (Toilet Brush) 1 na Hard bloom 1 (angalia picha hapo chini)
(x) Mzazi unashauriwa kumfungulia mwanao akaunti katika benki ya NMB ili kurahisisha utumaji wa fedha za kujikimu na nauli kipindi shule itakapofungwa.







**2.3 MICHANGO MBALIMBALI KWA SHULE ZA BWENI**

| Na | Aina ya Mchango | kiasi | Akaunti |
|---|---|---|---|
| 01 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000/= | 41101200041 RECURRENT ACOOUNT LOLIONDO SECONDARY SCHOOL |
| 02 | Tahadhari | 5,000/= | |
| 03 | Nembo | 5,000/= | |
| 04 | Kitambulisho | 5,000/= | |
| | **Jumla** | **80,000/=** | |

**3. 0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

0Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sh0eria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni Pamoja na;

**3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni lazima.
(iii) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).
(iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(vi) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapokuwa shuleni.
(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(ix) Kuwa na mavazi ya heshima, mavazi ya nyumbani na mitepesho hairuhusiwi kwa mwanafunzi.
(x) Kutunza mali za shule.
(xi) Ni marufuku mwanafunzi kumili vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.

**3.2 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

(i) Wizi
(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
(vi) Kufuga ndevu
(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
(viii) Uvutaji wa sigara
(ix) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
(x) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi.
(xi) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
(xii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(xiii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
(xiv) Kudharau Bendera ya Taifa
(xv) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
(xvi) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

**MUHIMU:-**

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilolopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum kutoka kwa Mkuu wa Shule (Msiba au Ugonjwa).

**4.0 VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU**

(i) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali.
(ii) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, mchango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
(iv) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni Pamoja na namba zao za simu.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI LOLIONDO.**

Saini ya Mkuu wa Shule: [signature]

Jina la Mkuu wa Shule: NEEMA G. MCHAU

Mhuri wa Mkuu wa Shule: HEAD MISTRESS
LOLIONDO SECONDARY SCHOOL
P.O BOX 61 LOLIONDO
EMAIL: loliondosec@yahoo.com

**NB:-** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- MKUU WA SHULE: **0754486342**
- MAKAMU MKUU WA SHULE**: 0769178802**
- MWANDAMIZI TAALUMA: **0786905178**
- MWANDAMIZI MALEZI: **0787443482**

## SHULE YA SEKONDARI LOLIONDO
## FOMU YA UTII NA TABIA NJEMA

Mimi: ______________________________________________ (Jina kamili)

Kidato cha ____________________________________Mwaka ________________

Natambua wajibu wangu kwa Taifa kama mwanafunzi na naahidi yafuatayo:-

A. Kwamba nitatii na kuwaheshimu viongozi wangu wote kuanzia ngazi ya darasa, Viranja, Walimu, Watumishi wote hadi Mkuu wa shule.

B. Kwamba nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.

C. Kwamba sitatoka nje ya mipaka ya shule wakati wa masomo labda tu kwa shuhguli maalumu baada ya kupata kibali maalumu kutoka kwa mwalimu au mkuu wa shule mwenyewe.

D. Kwamba kama nitashindwa kufuata hayo yote hapo juu hatua kali zichukuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kusimamishwa masomo.

Tarehe ____________________ ________________________________
Jina na saini ya Mwanafunzi

Tarehe ____________________ ________________________________
Jina na saini ya Mzazi/Mlezi

## SHULE YA SEKONDARI LOLIONDO
## FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI
## HABARI ZA MZAZI / MLEZI

1. Jina kamili la Mzazi /Mlezi ____________________________________________

2. Kazi ya Mzazi/Mlezi ________________________________________________

3. Anwani / Simu No. Mzazi / Mlezi ______________________________________

4. Nyumbani kwa Baba (Alikozaliwa Mtoto

Kijiji/Mtaa ________________ Kata-__________________Tarafa_______________

Wilaya___________________________ Mkoa____________________________

5. Anwani ya Mahali pa kazi ya Baba _____________________________________

6. Anwani ya mahali pa kazi ya Mama ____________________________________

7. Mtoto anaishi na (1) Baba tu. (2) Mama Tu. (3) Wazazi wote (4) Walezi "Kata isiyohusika"

8. Dini ya Baba _______________ Dhehebu_____________

Dini ya Mama______________ Dhehebu_____________

Dhehebu unalotaka mwanao alelewe ___________________________________

9. Anwani kamili ya nyumba ambapo mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo________________

10. Mimi ______________________________________________Baba/Mama/Mlezi wa____________________

Nathibitisha Taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na ninaahidi ushirikiano na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi namwenye bidii ya masomo. Pia naahidi kulipa Ada na michango ya shule kwa wakati na kwa ukamilifu ili kurahisisha huduma mbalimbali kwa mwanangu.

Tarehe ____________Jina na saini ya Mzazi/Mlezi ________________________

# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A**

TO: The Medical Officer,

…………………………………………………………………

…………………………………………………………………

…………………………………………………………………

**Mr & Mrs/Miss**

**………………………………………………………………………………………………………**

Please examine the above name as to his/her fitness mentally and for a full time Secondary Education. The examination should

include the following categories: (i-iii) each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of a defect.

Pregnancy (category iv) will also render a girl candidate in eligible for the Secondary Education.

i. (a) Eye-Sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech (e) Venereal Diseases
   (f) Leprosy (g) Epilepsy
ii. Neuroses
iii. Other serious
iv. Pregnancy

**Date: ………………………………………. Signature: ……………………………………..…….**

HEAD MISTRESS
LOLIONDO SECONDARY SCHOOL
P.O BOX 61 LOLIONDO
EMAIL: loliondosec@yahoo.com

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Gov. Office)

**PART B**

I have examined the above name and consider that he/she is physically and mentally fit/unit for full time Secondary Education.

i. (a) Eye-Slight ……………………………………..………………………………………….
   (b) Hearing ……………………………………………..…………………..………………

(c) Limbs …………………………………….……………………………………………..

(d) Speech …………………………………………..………………..…..………………….

(e) Venereal Diseases ……………………………..…………………..…………………

(f) Epilepsy …………………………………………………………………..……………….

(g) Leprosy ……………………………………………………………………...……………

ii. Neuroses ………………………………………...……………………………………………….

iii. Other Serious diseases ……………………………..………………………………………….

iv. Pregnancy …………………………………………...……………………………………..

**Date ………...…… Signature ……………………… Design …………………**